

TEACHER.CO.KE
KIDATO CHA PILI
MUHULA WA KWANZA, MWAKA 2022
KISWAHILI

ALAMA

MUDA: SAA 2

MAAGIZO: JIBU MASWALI YOTE

INSHA (ALAMA 20)

Andika kisa kitakachoonyesha ukweli wa methali hii: *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*

UFAHAMU

ALAMA 10

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Mwanadamu, ingawa kawaida huumbwa akiwa na afya bora wakati mwingine haiwi hivyo. Huenda **akakumbwa** na magonjwa aina mbalimbali; mengine madogo madogo na mengine makubwa. Magonjwa yale madogo madogo hayampi mtu wasiwasi mwingi bali akijua kuwa na magonjwa ya kumfishaa hupotelewa na raha kabisa, hushikwa na simanzi, hata anaweza akafa kabla ya siku zake kutimia.

Magonjwa madogo madogo (mepesi) ni kama mafua na kuumwa na kichwa, ilhalii magonjwa makubwa ni kama ukimwi, kipindunpindu na kifua kikuu.

Mtu akishikwa na maradhi hupotelewa na hamu ya chakula, wengine wakikiona tu huona kichefuchefu na kutapika. Maradhi **husononesha** na kumfanya mtu **akonde mithili ya ng'onda**. Wagonjwa wengine hushikwa na woga hasa wakijua kuwa watakata Kamba, wengine kati ya hawa **hyponda mali** yote waliyonayo kabla ya kuishiwa wa nguvu kabisa. Wale ambaa hupata nafuu humshukuru Mungu kwa kuwanusuru katika janga hilo kwani labda waliponea tundu la sindano.

Kila auguaye hushauriwa kwenda hospitali lakiini kuna wengine ambaa hata wakishauriwa kufanya hivyo hukataa katakata na mwisho **hujihasiri**. Watu wengi wakiwa na maradhi hatari kama ukimwi, tauni, ukoma, na kipindupindu hukimbiwa na marafiki. Marafiki hao huwa hawataki kuambukizwa. Baadhi ya wagonjwa hawa wakitengwa namna hiyo hutamani kujitia kitanzu.

Uchafu ni njia mojawapo kubwa inayowapatia watu magonjwa kama kichocho, kuhara damu, kipindupindu na hata minyoo wanaoweza kuwasumbua na kuleta safura. Inapasa kula chakula safi na kuwa nadhifu ili kujiepushe na shida kama hizo.

Magonjwa mengine hupatikana wakati mtu anapong'atwa na wadudu kama vile mbung'o ambao husababisha ugojwa na malale. Malaria husabibishwa na mbu. Hata kuna aina Fulani ya mbu wasabibishao ugonjwa wa matende.

Magonjwa kama surua, kifaduro na ugonjwa wa kupooza huwapata watoto na kuwaacha na matatizo **chungu nzima**, hasa wakikosa matibabu mapema. Kwa mfano, wakipoza miguu wanaweza kuwa viwete.

Magonjwa kama utapia mlo, kisunzi, ukosefu wa damu, upele, kuparara na kubambuka ngozi mwilini husababishwa na ukosefu wa chakula.

Maradhi husababisha **uzoroteshaji** wa maendeleo. Mgonjwa hawezi kuzalisha mali kwa kuwa atakuwa hana nguvu ya kufanya kazi. Isitoshe, watu wengine watakuwa wakimshughulikia na kazi zao hazitafanyika. Mara nyingi fedha nyingi hutumika kwa kumtibu mgonjwa huyo.

Juhudi zinafanywa **juu chini** ili kuamgamiza magonjwa yanayomaliza watu. Madawa chungu nzima yamegunduliwa na hospitali na zahanati zimejengwa kila sehemu ili wagonjwa watibiwe. Hata hivyo, juhudi hizi hazitoshi.

Walimwengu wataweza tu **kujiona** kuwa wana maendeleo kama watafaulu kuzivumbua dawa za kukomesha magonjwa yote yanayowasumbua. Wanatakiwa wasikate tamaa kwani huenda siku moja watafanikiwa. Yapasa waelewe kuwa palipo na nia hapakosi njia.

Maswali

1. Andika kichwa kinachofaa kueleza habari hii. (al. 1)

2. Taja aina **tatu** za magonjwa yaliyogusiwa katika kifungu hiki. (al. 3)

3. Maradhi husababisha hasara gani? (al. 3)

4. Taja njia tatu ambazo kwazo mtu anaweza kushikwa na maradhi. (al. 3)
-
-
-

5. Andika maana ya neno hili kama lilivyotumika katika taarifa hii. (al. 1)

Akakumbwa

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA **(ALAMA 20)**

- a. Tofautisha kati ya sauti hizi:

/m/ na /th/ (alama 1)

/o/ na /u/ (alama 1)

- b. Tenga silabi kwenye neno hili : ***muhtasari*** (alama 1)
-

- c. Onyesha majukumu mawili ya kiimbo kisha utolee mifano. (alama 2)
-
-
-

- d. Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 3)

timothy alienda shulen i tarehe 22 10 2021 akasoma kiswahili kingereza na hesabu

- e. Onyesha miundo yoyote miwili ya ngeli ya A-WA kisha utolee mifano. (alama 2)
-
-
- f. Tambua aina za maneno kwenye sentensi hii. (alama 2)
Huyu mdogo alienda shulenii.
-
-
- g. Onyesha viambishi awali , mzizi na viambishi tamati kwenye neno hili: *alipikiwa* (alama 2) -
-
-
- h. Nyambua vitenzi hivi kwenye kauli zilizowekwa kwenye mabano.
Kimbia (tendesha) (alama 1)
-
-
- i. Eleza maana ya sentensi. (alama 1)
-
-
- j. Taja aina zozote mbili za sentensi. (alama 1)
-
-
- k. Tambua Kundi Nomino na Kundi tenzi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
Mwanafunzi huyu mfupi atapewa zawadi kesho.

- i. Eleza maana ya fasihi. (alama 1)

- ii. Taja tanzu mbili kuu za fasihi. (alamu 1)

- iii. Andika tofauti zozote tano za tanzu ulizotaja hapo juu. (alamu 5)

- iv. Taja umuhimu wa fasihi kwa jamii. (alamu 3)

- a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

isimujamii

(alama 1)

sajili

(alama 1)

- b) Taja kaida zozote tatu za lugha

(alama 3)

- c) Orodhesha sifa zozote tano zinazotumiwa katika lugha ya shule.

(alama 5)